

**OFISI YA RAIS
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

Simu Na: +255 (026) 2963630
Nukushi: +255 (026) 2963629
Barua Pepe: ps@utumishi.go.tz

Tovuti: <http://www.utumishi.go.tz>



Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Utumishi,
S.L.P 670,
DODOMA.

DODOMA
29 Machi, 2024

TAARIFA KWA UMMA

**SERIKALI KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KIUTUMISHI KWA NJIA
YA KIELEKTRONI KUANZIA TAREHE 2 APRILI, 2024**

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma anapenda kuwajulisha waajiri na watumishi wa umma wote kuwa, kuanzia **tarehe 2 Aprili, 2024**, masuala yote ya kiutumishi yatafanyika kwa njia ya kielektroni kupitia mifumo mbalimbali ya Serikali.

Hii inatokana na kukamilika kwa ujenzi wa moduli mbalimbali ndani ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS). Moduli hizo ni pamoja na Uhamisho wa Vituo vya Kazi, Likizo, Ajira Mbadala na Kuajiriwa Upya katika Utumishi wa Umma.

Lengo la hatua hii ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma ikiwemo kusogeza huduma karibu na wananchi, kutatua kero za Watumishi wa Umma, kuweka uwazi na uwajibikaji wa Watendaji kwa wapokea huduma pamoja na kudhibiti udanganyifu.

Kwa msingi huo, masuala yote yanayohusiana na uhamisho wa kituo cha kazi, likizo za aina zote na mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha yatafanyika kwa njia ya kielektroni kupitia Mfumo tajwa kuanzia **tarehe 2 Aprili, 2024**. Kwa upande wa watumishi, maombi ya Mikopo kutoka Taasisi za Fedha, Uhamisho kutoka Taasisi moja kwenda nyingine na Likizo za aina zote zinatakiwa kufanyika kupitia dirisha la Watumishi *Portal* (ess.utumishi.go.tz).

Pamoja na masuala mengine, Waajiri wote ndani ya Utumishi wa Umma wanaelekezwa kushughulikia masuala yote yanayohusiana na Uhamisho wa Watumishi, Likizo za Watumishi, Ajira Mbadala (Replacement Permits) na Kuajiriwa Upya katika Utumishi wa Umma (Re-Engagement) kupitia Mfumo wa HCMIS (<https://hcmis.utumishi.go.tz>).

Kutokana na maelekezo hayo, hakutakuwa na ushughulikiaji wa masuala tajwa hapo juu yatakayofanyiwa kazi nje ya mfumo huo wa kielektroni.

Aidha, Katibu Mkuu anatoa wito kwa Waajiri ambao hawajaingia kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) wachukue hatua za kuingia katika Mfumo huo ili kuweza kupata huduma hizo. Aidha, watumishi wa umma wote ambao hawajajisajili kwenye Mfumo wa Watumishi *portal* (ess.utumishi.go.tz) wanakumbushwa kujisajili mapema ili masuala yao ya kiutumishi yaweze kufanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi kupitia Mfumo huo.

Ni wajibu wa waajiri na watumishi wa umma kutumia mifumo hii ili kurahisisha utendaji kazi na kuepusha malalamiko kwa watumishi kwa ustawi wa Taifa.



Mary L. Mwakapenda

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI